



KITUO CHA WAFANYAKAZI CHA WNYCOSH FAHAMU HAKI ZAKO

Kima cha Chini cha Mshahara

\$11.80/saa

Vibarua wa mashamba wana kima cha chini cha mshahara cha \$11.80/saa, na “mikataba ya wafanyakazi wa mashamba” inayobainisha jinsi mapato yanavyochumwa na hali ya mazingira ya kazi

Ratiba ya Vima vya Chini vya Mishahara*

Mwaka	Kima cha Chini cha Mshahara/saa
2020	\$11.80
2021	\$12.50

*Nje ya Mji wa New York

Wafanyakazi Wanaopewa Bahshishi

- Mapato ya \$7.85/saa na kiwango cha chini cha malipo cha \$3.95 kinachotolewa kama bahshishi **AU** kulipwa na mwajiri
- Kiwango cha bahshishi anachofaa kupata mfanyakazi au kinacholipwa na mwajiri huongezeka kulingana na kima cha chini cha mshahara
- Wafanyakazi wanaopewa bahshishi wako chini ya masharti ya ovataimu
- Wafanyakazi wanaopokea bahshishi au kiinua mgongo **huenda bahshishi zao zisidaiwe au kutiliwa mkazo kwa njia ya moja kwa moja au mbadala na mwajiri ua kwa niaba ya mwajiri**

Haki za Wafanyakazi wa Muda

Wafanyakazi wa muda wana haki ya:

- Kutobaguliwa na **wakala** wanaotumia na PIA mwajiri mwenyeji
- Kupokea mafundisho sawa au yanayolingana kuhusu usalama na wafanyakazi wa kudumu wa mwajiri
- Kima cha chini cha mshahara

Haki ya Mazingira Salama na yenye Afya

Chini ya sheria za afya na usalama za Marekani, una haki ya:

- Kufundishwa katika lugha unayoelewa
- Kuwa katika mazingira ya kazi yaliyo salama na yasiyo na hatari zinazotambulika
- Kupiga ripoti kwa msimamizi wako iwapo una shaka kuhusu afya na usalama
- Kuwasilisha malalamishi kwa OSHA kuhusu mazingira yasiyokuwa na usalama au afya njema
- Kukataa kufanya kazi unayodhania kwamba itakuweka kwenye hatari mara moja
- Kufahamu hatari zilizo katika mahali pa kazi
- Kutobaguliwa (kufutwa, kupewa kazi mbaya zaidi, n.k.) kwa kupiga ripoti kuhusu hali za hatari kwa usalama (Ulinzi kwa Watoa Taarifa)
- Kuweza kupata rekodi za vipimo vya afya na vipimo vya uchunguzi wa kuwepo kwa vifaa hatari katika mazingira ya kazi
- Kupata habari kuhusu visa vya majeraha au magonjwa vinavyotokea kazini

Ovataimu

Wafanyakazi wengi wanastahili kupata mara 1 ½ ya malipo yako ya kawaidakwa kila saa baada ya kuhudumu masaa 40 katika wiki

Masharti ya ovataimu huenda yasitumike kwa:

- Vibarua wa Mashamba
- Wafanyakazi Watendaji: wanaoweza kuajiri/kufuta na wanaoelekeza shughuli za kazi za wafanyakazi wawili au zaidi kwa mara nyingi
- Wafanyakazi Wataalamu: walio na digrii ya miaka 4 au ambao kazi zao ni za ubunifu
- Wafanyakazi Wasimamizi: wanaofanya maamuzi ya busara na huru au ambao kwa wakati mwingi hufanya kazi za ofisi/kazi za uwandani zisizo za mikono zinazohusiana moja kwa moja na sera za usimamizi

Marudio ya Kupokea Malipo

Ni lazima wafanyakazi wengi wapate malipo ya kazi zao ndani ya siku 7 baada ya kipindi walichofanya kazi

Haki ya Kutobaguliwa

Sheria ya Title VII na Kitengo cha Haki za Binadamu cha Jimbo la New York hulinda wafanyakazi kutokana na ubaguzi.

Makundi Yanayolindwa Kutoka kwa Ubaguzi

- Asili
- Rangi
- Nchi ya Asili
- Dini
- Jinsi
- Ulemavu
- Utambulisho wa Hisia za Kimapenzi
- Hali ya Uanajeshi
- Hali za Kijeni Zinazobainisha Mielekeo
- Hali ya Familia
- Hali ya Ndoa
- Halia ya Kuathiriwa katika Vita vya Kinyumbani
- Ujauzito
- Shughuli za Kisiasa (nje ya kazi)
- Shughuli za Kujiburudisha (nje ya kazi)
- Uanachama katika Miungano

Ulinzi wa Watoa Taarifa

Ni hatia kumwadhibu au kumfuta mfanyakazi kwa kutoa au kuwasilisha malalamishi kwa wakala yeyote wa serikali

Mwajiri **hafai** kuwaadhibu wafanyakazi kwa kushtaki mwajiri kwa wakala wa serikali kwa nia njema

Mwajiri huenda akatakiwa kuwajibika kisheria iwapo atalipiza kisasi kwa:

- Kufuta/Kuachisha kazi
- Kuweka mwajiri kwenye orodha ya watu wabaya
- Kushusha cheo
- Kunyimwa malipo ya Ovataimu/ Kupandishwa Cheo
- Kukosa kuajiriwa/kuajiriwa tena
- Kutia woga
- Kutoa vitishoi
- Kupunguza Malipo
- Kupunguza Masaa ya Kazi
- Kuadhibu
- Kutotoa mafao
- Kuteua mfanyakazi kwa kazi nyingine kunakoathiri uwezekano wa kupandishwa cheo

Haki ya Malipo kwa Wafanyakazi

Ukijeruhiwa ukiwa kazini:

- Una haki ya kuwa na bima ya mishahara ya wafanyakazi, hata ikiwa malipo yako si rasmi au hayarekodiwi
- Unafaa kujaza fomu ya madai ya Wafanyakazi au ya C-3 kupitia mwajiri wako au unaweza kupokea usaidizi kupitia Simu ya Moja kwa Moja ya Kituo cha Wafanyakazi cha WNYCOSH: **(716) 206-3550**